JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATAKA - TUNDURU RUVUMA



CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu.......................**

**Mkuu wa Shule: 0753412885/0621981409**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0683750480/0620118965**

**Matron/Patron: 0624214557/0685973126**

**Shule ya Sekondari : MATAKA**

**S.L.P: 175 TUNDURU.**

**Tarehe ........................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P .........................................**
**................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATAKA HALMASHAURI YA TUNDURU MKOA RUVUMA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi aliyochaguliwa.
Shule ya Sekondari MATAKA ipo umbali wa Kilometa TATU (03) Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa TUNDURU Usafiri wa kutoka stendi kuu,nauli ni Shilingi 2000/= kwa pikipiki na Shilingi 5000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe................. Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**



CamScanner

## 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Suruali 02 na tai 02 za rangi ya ugolo
ii. Mashati meupe mikono mirefu pair 2 (tetron) zenye kola shingoni na siyo zenye kubana, na kizibao rangi ya ugolo.
iii. Sare ya Michezo ni bukta na tisheti za blue jozi 2,viatu vya michezo (raba), tracksuit za rangi ya blue kwa wavulana.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta ya ugolo (mbili) Nguo za kushindia ni suruali mbili nyeusi na T-shirt 2 za blue zisizo na maandishi. (*shamba dress*)
viii. Tisheti (yenye kola) 01 sehemu ya sare ya shule rangi ya kijivu au unaweza kuipata shuleni kwa Tsh 15000/=

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 07 counterbook.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe ft 2.5 ,mto na foronya rangi ya blue.
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue. , blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
ix. Kwanja 1 kwa wote ,pia kwa HKL waje na sabuni ya kudekia chooni ya maji lita 5, HGFa wanatakiwa kuja na brash ngumu na laini ya kudekia chooni, HGK anatakiwa kuja na brash ya kusugulia sinki la chooni na fagio ya kufagilia nje, HGL waje na jembe, na HGLi waje na mopa ya kusukumia maji na fagio ya kufagilia nje.

## 2.3 Michango mbalimbali

**Shule ya Bweni ya Sekondari Mataka - Tunduru.**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB. Michango hii inatakiwa iwekwe kwenye akaunti ya shule 70901100053 jina la akaunti ni MATAKA SECONDARY SCHOOL. Benk ni NMB**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na



CamScanner

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;



CamScanner

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**

**Saini ya Mkuu wa Shule :** ............................................

**Jina la Mkuu wa Shule :** **NIVER R MBUMDA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ............................................

HEADMASTER
MAIKA... ...DARY
P.O.BOX 175

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0753412885/0616003885**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0629125366/0752082305**
- **Mwandamizi Taaluma : 0628880967**
- **Mwandamizi Malezi : 0624214557**

Medical examination form. Form No 3

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
TUNDURU DISTRICT COUNCIL

RUVUMA REGION
PHONE NO. +255(0) 753412885

Mataka secondary School,
P.O.BOX 175
TUNDURU.
Date : ……………………………

Ref .No. MDSS/UKV /99 / VOL 1/ 2023
To Medical Officer
……………………………………………………
……………………………………………………
,………………………………………………………

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please Examine ………………………………………………as to his fitness for pursuing secondary school studies in this school.

General condition of his health:

Eye/ Vision ………………………………………………………………
Ears / Hearing ……………………………………………………………
Mouth / Speech……………………………………………………………
Nose / Smell ………………………………………………………………
Blood group ………………………………………………………………
Stool ………………………………………………………………………
Urine ………………………………………………………………………
HB% ………………………………………………………………………
Leucocytes …………………………………………………………………
E.S.R ………………………………………………………………………
Others ………………………………………………………………………

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named student. Consider and recommend him fit/ not fit for studies. Special medical recommendation. (if any)

……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

Date: ……………………………………… Signature…………………………
Designation ………………………………………

CamScanner